

# WILAYA YA NYANG'HWALE.

## TANGAZO LA NAFASI ZA KUKIMBIZA MWENGE WA UHURU KIWILAYA.

30/06/2023

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale anawatangazia wananchi wote walio na sifa za kukimbiza Mwenge wa Uhuru Kiwilaya kwa mwaka 2023 kuomba nafasi hiyo.

### SIFA ZA MKIMBIZA MWENGE WA UHURU.

1. Awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 35
2. Awe Mkakamavu, Mvumilivu, Mwadilifu na Mzalendo.
3. Awe na afya njema ya kimwili na kiakili
4. Awe na nidhamu isiyoweza kutiliwa shaka
5. Awe na uwezo wa kutunza siri
6. Awe hajawahi kushitakiwa, kufungwa ama kupatikana na kosa lolote la jinai
7. Awe anatoka katika Taasisi ya Umma/Serikalini, Sekta Binafsi ama anaye jiajiri.
8. Awe na Elimu ya kuanzia darasa la saba na anajua kusoma na kuandika.

Maombi yote yatumwe kwa Anuani ya :-

**MKUU WA WILAYA,  
S.L.P 181,  
NYANG'HWALE.**

- Kwa waombaji ambao ni waajiriwa wa Taasisi za Umma wahakikishe maombi yao yanapitishwa na Wakuu wao wa Taasisi na kwa wale ambao si waajiriwa wa Serikali maombi yao yapitishwe na Afisa Mtendaji wa Kijiji anachotoka mwombaji.
- Maombi yote yaambatanishwe na picha moja ya passport size, Cheti cha Daktari, Cheti cha Kuzaliwa na namba ya simu.
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **06/07/2023** saa tisa na nusu alasiri maombi yote yawasilishwe ofisi ya Mkuu wa Wilaya .



Manyoni E. N

**KAIMU KATIBU TAWALA WILAYA  
NYANG'HWALE.**

**KATIBU TAWALA WA WILAYA  
NYANG'HWALE**